

Swahili

Mwaliko

Unakaribishwa kutoa maoni yako kuhusu kuwepo kwako katika programu ya utangulizi

Habari?

Washiriki wote wa programu ya utangulizi hapa Norway wanaalikwa katika utafiti wa kitaifa.

Ni matumaini yetu kwamba utaitumia fursa hii kujibu maswali ili kutoa maoni yako yanayohusu ushiriki wako katika programu ya utangulizi. Yapo majibu ya kuchagua.

Utafiti huu umetayarishwa na wizara ya ujumuishaji na utofauti wa watu.

Tunahitaji uzoefu wako ili manispaa yako iweze kukupatia fursa iliyo bora zaidi pamoja na wengine mnaoshiriki pamoja katika programu ya utangulizi.

Jambo la muhimu ni kwamba uwe mkweli na muwazi katika kutoa majibu yako ili kwamba tuweze kupata maelezo ya mambo ambayo ungependa yaboreshwe. Kwa mfano, unaweza kuulizwa ikiwa unaridhishwa na mafunzo unayopewa, na ikiwa unafurahia kuwepo katika programu, na kama kuna mambo ambayo si mazuri pia katika programu.

Utafiti huu ni wa hiyari na unaweza kutumia dakika 30 katika kujibu majibu ya utafiti huu. Utafiti huu ni wa siri. Majibu yako hayawezi kujulikana kuwa ni wewe binafsi uliyejibu. Wafanyakazi wa IMDi katika mradi huu pamoja na watafiti maalumu watakuwa na uwezo wa kuyasoma majibu na watatunza majibu yote kwa siri. Hakuna mfanyakazi wa manispaa wala wengine watakaokuwa na uwezo wa kuyasoma majibu utakayotoa.

Manispaa yako itakupatia nyezo za kukuwezesha kuingia katika utafiti huu.

Unaweza kuchagua lugha katika utafiti huu. Tumia vitufe pale chini kwenye ukurasa huu. Maswali yote na majibu ya kuchagua yapo katika maandishi na sauti. Tumia kitufe cha sauti ikiwa unataka kusikia maswali na majibu mbalimbali.

Unapaswa kujibu maswali yote kwa mpigo

Asante kwa kujiunga na utafiti huu

Wasalaam,

Integrerings- og mangfoldsdirektoratet